




Isaya ni nani?

Kwenye Kitabu cha Mormoni, tunasoma maneno ya mtu aliyeitwa Isaya. Isaya alikuwa nabii wa Agano la Kale. Aliishi zamani kabla Yesu Kristo hajazaliwa.



Isaya alifundisha kuhusu maisha ya Yesu Kristo. Alisema kwamba Yesu angeleta amani katika ulimwengu. Alifundisha kwamba Yesu angekufa, na kufufuka na kurudi tena duniani siku moja.



Mamia ya miaka baadaye, Nefi aliandika maneno ya Isaya katika Kitabu cha Mormoni ili kutufundisha kuhusu Yesu Kristo. Wakati Yesu alipowatemblea Wanefi, Yeye alishiriki maneno ya Isaya. Yeye alituomba tujifunze maneno haya. Tunapojifunza maneno ya Isaya, tunaweza tukauhisi upendo wa Mwokozi na kuja karibu Naye. ●

MAJIBU: MATANO, NIWA, KILA MFTU

VIELELEZO NA BEN SIMONSEN

Changamoto ya Maandiko

Soma 2 Nefi 19:6. Kuna majina mangapi ya Yesu katika mstari huu?

Ni kiumbe gani kilitokea ili kuonyesha kwamba Roho Mtakatifu alikuwa katika ubatizo wa Mwokozi?

Dokezo: 2 Nefi 31:8

Ni nani atafufuliwa?

Dokezo: Alma 11:44

Ninaweza Kusoma Kitabu cha Mormoni!

Baada ya kusoma, paka rangi sehemu ya picha. Unaweza kusoma maandiko haya yanayoenda sambamba na usomaji wa kila wiki kutoka *Njoo, Unifuate*.

- Wiki ya 1:** 2 Nefi 11:2
- Wiki ya 2:** 2 Nefi 24:3
- Wiki ya 3:** 2 Nefi 26:23-24
- Wiki ya 4:** 2 Nefi 32:5
- Wiki ya 5:** 2 Nefi 9:13



Isaya alifundisha kwamba Yesu ni "Mfalme wa Amani" (2 Nefi 19:6). Chora au piga picha ya kitu fulani ambacho hukusaidia uhisi amani. Tuma picha ya kitu hicho kwa *Rafiki*!

Tazama jalada la nyuma kujuu jinsi ya kufanya hivyo.